ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaibah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.

47.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe.
48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53.Mhe. Asha Bakari Makame	Uteuzi wa Rais.
54. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
55.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
57.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
58.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
59.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
60.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
61Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
62.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
63.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
64. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
65.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
66.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.

67.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
68.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
69.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
70. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
71.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
72.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
73.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
74.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
75.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
76.Mhe. Saleh Ramadhan Feruz	Uteuzi wa Rais.
77.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
78..Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
79.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
80.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Ishirini na Tano – Tarehe 16 Julai, 2010

(Mkutano ulianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

KUAHIRISHWA BARAZA

Mhe. Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha kuendesha shughuli za Baraza lako tukufu kwa ufanisi. Pili, nakushukuru wewe Mhe. Spika kwa kuongoza mkutano huu kwa hekima na busara. Halikadhalika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu kwa kuuliza maswali mazuri kuhusu utendaji wa shughuli za serikali na kujadili bajeti mbali mbali zilizowasilishwa katika mkutano wa bajeti ya mwaka huu. Mwisho, nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri kwa kuyajibu vizuri maswali yote yalioulizwa na kutoa ufafanuzi mzuri wa hoja za Waheshimiwa Wajumbe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama mnavyojua Rais Dkt. Amani Karume amemaliza muda wake katika kipindi cha miezi minne. Kwa hiyo hotuba yangu ya mwaka huu itaeleza mafanikio ya uongozi wake katika kipindi chake cha pili na cha mwisho, yaani kuanzia 2005 hadi 2010 ili sisi Waheshimiwa Wajumbe pamoja na wananchi tuweze kujua wapi tunatoka, tulipo na tunakokwenda ili kuweka misingi madhubuti kwa serikali inayokuja.

Mhe. Spika, kufuatia ushindi wa Chama cha Mapinduzi katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2005, CCM ilikabidhiwa madaraka ya kuunda serikali chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Amani Karume. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Dkt. Karume imepiga hatua kubwa katika kuleta maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. *(Makofi)*

Katika medani ya kisiasa, Zanzibar imeendelea kuwa na utulivu kufuatia maridhiano yaliyofikiwa tarehe 05 Novemba 2009 kati ya Rais Karume mwenyewe na Maalim Seif Sharif Hamad, Katibu Mkuu wa CUF. Hali hii imewasaidia wananchi kujenga maelewano na ushirikiano katika kutekeleza miradi ya maendeleo na ustawi wa jamii kama vile Kampeni za Kitaifa dhidi ya Malaria, uhifadhi wa mazingira, miradi ya *TASAF*, pamoja na kujiunga na vikundi vya kuweka na kukopa (*SACCOS*).

Mhe. Spika, utulivu wa kisiasa uliopo Zanzibar pia umelisaidia Baraza la Wawakilishi, ambapo ni chombo muhimu katika kukuza demokrasia na madaraka ya umma, kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Kwa hivyo, sote ni mashahidi kwamba kumekuwa na maelewano makubwa sana kati ya Wajumbe kutoka kambi mbili hizi za kisiasa. *(Makofi)*

Kwa mfano, Waheshimiwa Wajumbe kutoka Kambi ya Upinzani wamekuwa wakikosoa na kusifu kwa heshima pale inapostahiki. Kwa kweli hii ni dalili njema kwa maendeleo ya demokrasia kwa siku zinazokuja. *(Makofi)*

Wajumbe wa Baraza hili wameendesha shughuli zao kwa ushirikiano wa hali ya juu sana. Vile vile Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar nayo imefanya kazi vizuri katika uandikishaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Hivi sasa Tume ya Uchaguzi inaendelea na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu ujao na tayari imeshaanza kuwapatia wananchi Vitambulisho vya Kupiga Kura, ili waweze kushiriki katika Kura ya Maoni pamoja na Uchaguzi Mkuu mwaka ujao.

Mhe. Spika, waasisi wa Muungano waliamua kuziunganisha nchi zetu mbili, yaani Tanganyika na Zanzibar, ili kuimarisha umoja na maendeleo. Ili kufikia azma hiyo Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimekuwa zikishirikiana kikamilifu katika utekelezaji wa miradi ya uzalishaji mali na kijamii kupitia programu na miradi mbali mbali ya pamoja.

Kutokana na Agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Serikali zetu kukutana, kwa ajili ya kutatua kero za Muungano. Vikao sita vimefanyika chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein. Katika vikao hivi masuala mbali mbali yamejadiliwa na kupatiwa ufumbuzi. Vikao vitaendelea kujadili na kuyapatia ufumbuzi masuala yaliyobaki hasa suala la Hisa za Zanzibar katika Benki Kuu ya Tanzania na ugawaji wa mapato ya taasisi za Muungano kati ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, ukuaji wa uchumi umeongezeka kutoka asilimia 4.9 mwaka 2005 hadi asilimia 6.7 mwaka 2009. Ukuaji huu umechangiwa na sababu kadhaa zikiwemo kuongezeka kwa uzalishaji wa Sekta ya Kilimo, kukua kwa Sekta ya Ujenzi, kupanuka kwa thamani ya shughuli za biashara, kuongezeka cha uwekezaji na ongezeko la idadi ya watalii nchi.

Ukuaji huu wa uchumi umeongeza pato la Taifa kutoka shilingi 394,900 milioni mwaka 2005 hadi shilingi 878,403 milioni mwaka 2009. Wastani wa pato la mtu binafsi pia limeongezeka kutoka shilingi 368,000 mwaka 2005 hadi shilingi 728,000 mwaka 2009. Vile vile ukuaji wa rasilimali umeongezeka kutoka

shilingi 76,178 milioni mwaka 2005 hadi shilingi 175, 877 milioni mwaka 2009 kutokana na kukua kwa uwekezaji katika sekta za miundo, biashara na ujenzi. Kiwango cha uwekezaji binafsi nacho kimepanda maradufu kutoka dola za kimarekani 120.91 milioni 2005 hadi 1,296.8 milioni mwaka 2008.

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio yaliyoainishwa hapo juu mfumko wa bei umepanda kutoka asilimia 9.7 mwaka 2005 hadi asilimia 20.6 mwaka 2008. Hali hii imesababishwa na uzalishaji mdogo usiokidhi mahitaji ya chakula hapa Zanzibar, kupanda kwa bei ya chakula na bidhaa za petroli duniani, kushuka kwa thamani ya sarafu na msukosuko wa uchumi duniani. Hata hivyo, katika mwaka 2009 kasi ya mfumko wa bei ilipungua hadi kufikia asilimia 8.9 kufuatia uzalishaji mzuri wa mazao ya kilimo na kushuka kwa bei za vyakula na bidhaa za petroli duniani.

Mhe. Spika, ukusanyaji wa mapato una umuhimu mkubwa katika kugharamia shughuli za Serikali. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, ukusanyaji halisi wa mapato ya ndani umeongezeka kutoka wastani wa shilingi bilioni 5.8 kwa mwezi sawa na shilingi bilioni 70 kwa mwaka 2005/2006 hadi kufikia shilingi bilioni 12.5 kwa mwezi sawa na shilingi bilioni 150 kwa mwaka 2009/2010.

Serikali inaendelea kuchukua hatua mbali mbali za kisheria, kiutawala na kiutendaji, ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani. Matumizi ya Serikali nayo yameongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na mahitaji ya huduma za jamii na shughuli za serikali kwa ujumla. Matumizi ya kawaida yameongezeka kutoka shilingi bilioni 90 kwa mwaka 2005/2006 hadi kufikia shilingi bilioni 168 kwa mwaka 2009/2010.

Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo ya jumla sasa nitaeleza mafanikio yaliyopatikana katika kila sekta ya maendeleo.

SEKTA YA KILIMO

Sekta ya Kilimo inatoa mchango mkubwa katika kukuza pato la taifa na ajira. Ukuaji wa sekta hii unategemewa sana kuinua uchumi na kupunguza umasikini. Sekta hii inajumuisha kilimo cha mazao, mifugo, uvuvi na mazao ya baharini, maliasili za misiatu na mazingira. Mchango wa sekta hii katika pato la taifa umepanda kutoka asilimia 23.4 mwaka 2005 hadi asilimia 30.8 mwaka 2009.

Mhe. Spika, kupitia miradi ya *PADEP*, *MANCEMP* na *TASAF* wafugaji, wavuvi na wakulima wameweza kuongeza tija na uzalishaji. Serikali imeelekeza juhudi kubwa katika kutoa huduma za utafiti wa mazao, huduma za elimu kwa wakulima, kuimarisha miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji, kukuza

mwamko wa uhifadhi wa mazingira, kuwapatia wavuvi vifaa vya uvuvi, ili kuwawezesha kuvua kwenye kina kirefu cha maji.

Kutokana na utekelezaji wa miradi na programu kadhaa zilizoainishwa hapo juu, uzalishaji wa mazao ya chakula umeongezeka. Kwa upande wa Sekta ya Uvuvi, thamani ya samaki waliovuliwa imeongezeka kutoka shilingi 24,671 milioni mwaka 2005 hadi shilingi 47.7 bilioni mwaka 2009.

SEKTA YA BIASHARA NA VIWANDA

Mhe. Spika, katika kipindi hiki Serikali imeanzisha Baraza la Biashara lenye wajumbe kutoka Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, ili kutatua matatizo yanayowakabili wafanya biashara. Serikali pia imetayarisha Sera ya Biashara, pamoja na kutoa mafunzo ya ujasiriamali, usindikaji wa mazao ya kilimo na kuongeza thamani ya mazao na bidhaa za kilimo kwa wajasiriamali 250. *(Makofi)*

Vile vile serikali imeratibu ushiriki wa vikundi mbali mbali vya wajasiriamali katika maonyesho ya kibiashara ndani na nje ya nchi. Halikadhalika, serikali imeandaa Sera ya uendelezaji wa viwanda vidogo vidogo na vya kati ili kukuza uzalishaji wa bidhaa mbali mbali kwa ajili ya masoko ya ndani na nje. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, serikali imeimarisha miundombinu na vivutio vya utalii, ili kuiendeleza sekta ya utalii na kuwavutia watalii wengi zaidi kuja Zanzibar. Serikali imechukua hatua mbali mbali katika kuitangaza Zanzibar kupitia magazeti na majarida ya kimataifa, tovuti na mitandao, matangazo ya televisheni na vyombo vya habari vya kimataifa. Serikali pia imeimarisha mitaala ya Chuo cha Maendeleo ya Utalii, ili kiweze kutoa mafunzo katika ngazi ya diploma.

Mhe. Spika, kama mnavyoelewa miundombinu ya kiuchumi ni muhimu katika kukuza uchumi na ustawi wa jamii. Kwa upande wa ujenzi wa barabara jumla ya kilomita 137 zimejengwa kwa kiwango cha lami Unguja na Pemba. Hivi sasa serikali pia inakamilisha maandalizi ya ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 132.7 Unguja na Pemba.

Kwa upande wa miundo mbinu ya usafiri wa baharini, serikali imekamilisha ujenzi wa bandari ya Malindi iliyogharimu jumla ya shilingi bilioni 41. Vile vile tumekamilisha matengenezo ya bandari ya Wesha, Pemba kwa gharama ya shilingi 358.7 milioni. Serikali sasa inaelekeza nguvu zake katika kufanya matengenezo ya Gati ya Mkokotoni, Unguja ili kupunguza msongomano wa vyombo vya mizigo na abiria katika bandari kuu ya Malindi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika usafiri wa anga, huduma za ndege zimeendelea kuimarishwa katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Zanzibar na Karume, Pemba. Viwanja hivi vimehudumia safari za ndege 158,026 ambapo kati ya hizo 18,519 ni za kimataifa na ndege 139,509 ni za ndani. Huduma kwa abiria nazo zimeongezeka kutoka abiria 414,810 kwa mwaka 2005 hadi 483,202 kwa mwaka 2009.

Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Zanzibar una uwezo wa kuhudumia ndege aina ya Boeing 767-300 na Airbus 330-200 zenye uwezo wa kubeba abiria 300. Kazi ya ukarabati wa barabara ya kurukia na kutulia ndege katika uwanja huu zinaendelea chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia kwa thamani ya shilingi bilioni 42. Serikali ina mpango wa kujenga jengo jipya la abiria. Hivi sasa serikali tayari imeshatiliana saini na Kampuni ya "*Beijing Construstion Company Ltd*" ya China kutekeleza ujenzi huo kupitia mkopo nafuu kutoka Benki ya *EXIM* ya China. *(Makofi)*

SEKTA YA ELIMU

Mhe. Spika, shabaha ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kujenga jamii iliyoelimika kama inavyosisitizwa na malengo ya Dira ya Maendeleo ya 2020. Serikali inachukua hatua mbali mbali kuimarisha ubora wa elimu ikiwemo kufundisha walimu wenye ujuzi, kusambaza vitabu na vifaa vya maabara. Ili kuongeza fursa za elimu ya sekondari Serikali yetu imetiliana saini na Benki ya Dunia mkataba wa ujenzi wa skuli 19 za sekondari za kisasa katika wilaya 10 za Unguja na Pemba. Ujenzi huu unategemea kugharimu dola za kimarekani 42 milioni.

Kwa upande wa Elimu ya Juu, fursa za elimu ya juu, sayansi na teknolojia zinaongezeka kutokana na wimbi kubwa la wanafunzi wanaojiunga na Vyuo Vikuu vya Zanzibar vya Zanzibar na vilivyo nje ya Zanzibar. Idadi ya waliojiunga na vyuo vikuu vya Zanzibar imeongezeka kutoka wanafunzi 1,142 mwaka 2005 hadi 3,572 mwaka 2009. Vile vile serikali imeanza ujenzi wa majengo ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, ili kuongeza fursa za elimu ya juu kwa vijana wa Zanzibar. *(Makofi)*

SEKTA YA AFYA

Mhe. Spika, afya bora ni miongoni mwa mambo yaliyopewa umuhimu mkubwa na Serikali tangu Mapinduzi ya 1964. Serikali imeifanyia ukarabati Hospitali ya Mnazimmoja pamoja na kuiwekea vifaa vya kisasa, kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa maradhi mbali mbali. Serikali pia imeanzisha mpango wa kutoa elimu ya afya, ili kuwakinga wananchi na maradhi mbali mbali.

Mhe. Spika, **s**erikali imechukua hatua madhubuti za kuutokomeza ugonjwa wa malaria kwa kupitia Kampeni ya **KATAA MALARIA.** Serikali imefanikiwa kupunguza ugonjwa wa malaria kutoka wastani wa asilimia 40 mwaka 2005 hadi asilimia 1 hivi sasa. Haya ni mafanikio makubwa katika sekta ya afya. Serikali pia inaendeleza na Kampeni za kupambana na kipindupindu na pepopunda.

Kwa upande wa kuwalinda watoto dhidi ya maradhi ya surua, serikali imefanikisha kutoa chanjo ya surua kwa watoto wenye umri wa miezi sita hadi miaka 10 kwa asilimia 95. Pia tumeongeza kiwango cha utoaji wa matone ya Vitamin "A", pamoja na kupunguza ongezeko la watoto wanaoathiriwa na minyoo. Halikadhalika, Serikali inaendelea kutoa huduma za kupambana na maradhi mbali mbali kama vile kisukari, sindikizo la damu, maradhi ya moyo na kansa.

Mhe. Spika, kwa upande wa huduma za uzazi salama na hifadhi ya mama na mtoto, serikali imekamilisha na kuzindua mkakati wa kupunguza vifo vya mama na mtoto. Katika utekelezaji wa mkakati huo wodi mpya ya wazazi ilifunguliwa katika Hospitali ya Mnazimmoja pamoja na kutawanywa huduma hizo katika vituo kumi na moja Unguja na Pemba. Vile vile serikali imewapatia wahudumu wa afya 27 wamepatiwa mafunzo ya kutoa huduma hizo katika sehemu zao za kazi.

Mhe. Spika, maradhi ya UKIMWI ni miongoni mwa changamoto zinazoikabili sekta ya afya hapa Zanzibar. Hivi sasa kiwango cha maambukizi kinaongezeka kwa kasi miongoni mwa makundi maalum kama vile watumiaji wa madawa ya kulevya na watu wanaojishughulisha na ngono za jinsia moja.

Katika kukabiliana na hali hii vituo vya kuchunguza virusi vya UKIMWI vimefunguliwa na huduma za kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda mtoto zimeimarishwa. Huduma ya tiba kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI zinatolewa katika hospitali mbali mbali Unguja na Pemba. Serikali inaendelea kutoa huduma za chakula majumbani kwa wagonjwa wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

Mhe. Spika, mpaka kufikia mwaka 2010, huduma za maji zimeimarika sana. Katika maeneo ya mijini huduma za upatikanaji maji zimefikia asilimia 70 na asilimia 60 kwa vijijini. Mafanikio haya yamepatikana kutokana na utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maji ikiwemo mradi wa maji wa Mkoa wa Mjini Magharibi unaofadhiliwa na Serikali ya Japan, *TASAF*, *EU*, *Red Cross*, *UNICEF*, pamoja na *UNDP*.

Vile vile Benki ya Maendeleo ya Afrika na *UNHABITAT* wamekubali kuipatia serikali msaada wa kutekeleza miradi mingine 12 ya maji safi na usafi wa mazingira. Miradi hii ina lengo la kuimarisha huduma za upatikanaji maji safi katika miji ya Chake Chake, Wete na Mkoani. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Sekta ya Nishati ni muhimu katika kukuza uchumi na ustawi wa jamii. Katika jitihada za kuwapatia wananchi huduma hizo serikali imekamilisha mradi wa kupeleka umeme Pemba kutoka Tanga uliogharimu dola za kimarekani 65 milioni. Serikali pia tayari imeshatiliana saini na Kampuni ya VISCAS mkataba wa kutengeneza waya wa umeme kwa ajili ya kusafirisha umeme megawati 100 kwa ajili ya kisiwa cha Unguja. Serikali pia imeshanunua majenereta 32 yenye thamani ya dola milioni 13 kwa ajili ya umeme wa akiba. Majenereta haya yana uwezo wa kuzalisha *megawatt* 25 ikiwa sawa na asilimia 50 ya mahitaji ya umeme Zanzibar. *(Makofi)*

UWEZESHAJI WA WANANCHI

Mhe. Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (*TASAF*) umeanzishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili kuwawezesha wananchi katika jitihada zao la kupunguza makali ya umaskini. Mfuko wa *TASAF* unafadhiliwa na Benki ya Dunia. Ili kutekeleza miradi ya *TASAF* Zanzibar imetengewa dola 7.9 milioni.

Utekelezaji wa awamu ya pili ya *TASAF* unafanywa kwa kupitia mifuko mitatu – Mfuko wa Taifa wa Kijiji, Mfuko wa Mradi wa Ukanda wa Bahari na Mfuko wa Tume ya UKIMWI. Kati ya fedha hizo mfuko wa kijiji dola 2.5 milioni, *MACEMP* dola 3.6 milioni na Tume ya UKIMWI dola 1.8 milioni. Serikali imetekeleza jumla ya miradi 632 yenye thamani ya shilingi bilioni 9.4. Miradi iliyotekelezwa ni miradi ya jamii, makundi maalum, uhakika wa chakula na mapambano dhidi ya UKIMWI na mazingira.

MFUKO WA HIFADHI YA JAMII

Mhe. Spika, katika kuwajengea hatma njema wafanyakazi baada ya kustaafu serikali ilianzisha mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (*ZSSF)*, ambao hadi kufikia mwezi wa Juni 2010 wanachama 58,283 wamejiunga kutoka Serikalini, Mashirika ya Umma na wengine kutoka Sekta Binafsi. Jumla ya shilingi bilioni 42,363 zimekusanywa kutoka kwa wanachama katika kipindi cha 2005-2010. Mfuko umewekeza katika miradi ya uchumi na biashara, ili kuongezea mfuko uwezo.

Mhe. Spika, mpaka kufikia Juni, 2010 jumla ya shilingi bilioni 57.5 zimewekezwa katika miradi mbali mbali. Kwa upande wa mafao kwa

wanachama mfuko huu hadi kufikia mwezi wa Juni, 2010 umewalipa mafao wanachama 7,133 yenye thamani ya shilingi bilioni 8.0. Vile vile serikali imeanzisha Mfuko wa Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi. Mfuko huu umezinduliwa na Rais Karume mwezi wa April, 2008. Mfuko huu hadi kufikia mwezi wa Machi 2010, umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi 1,314,640,000 kwa watu binafsi, vikundi vya kuweka na kukopa na vikundi vya kiuchumi 53. *(Makofi)*

TAASISI ZA FEDHA

Mhe. Spika, katika kupunguza umasikini Taasisi za Fedha nchini zimekuwa mstari wa mbele kutoa mikopo kwa wananchi. Benki ya Watu wa Zanzibar imetoa mikopo ya shilingi bilioni 51.6 kwa wafanyakazi 30,716 wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Taasisi za Muungano. Benki hiyo pia imetoa mikopo ya shilingi bilioni 12.78 kwa wafanyabiashara. Benki ya Posta Tawi la Zanzibar limetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 2.17 kwa wafanyakazi wapatao 1,798. Hapana shaka mikopo hii imewasaidia sana wafanyakazi kuanzisha miradi ya biashara na ujenzi wa nyumba bora za kuishi.

Mhe. Spika, mtakumbuka kuwa kwa muda mrefu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa ikikabiliwa na tatizo la malipo ya wastaafu siku za nyuma. Kwa bahati njema serikali sasa imeweza kuondoa kero hii kwa kulipa malimbikizo ya madeni ya viinua mgongo. Hadi kufikia Juni, 2010 serikali tayari imeshawalipa wastaafu wote waliokuwa wakiidai serikali. Jumla ya shilingi bilioni 28 zimetumika kuwalipa wastaafu 6,040 kutoka mwaka 2005 – 2010. Hali ya sasa inaridhisha kwani mara tu mfanyakazi anapostaafu anapatiwa haki zake zote bila ya ucheleweshaji wowote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kuwa Serikali ya Rais Karume inamaliza muda wake nimeona ni busara pia nieleze mafanikio ya serikali katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, ili tuweze kujua kwa kiasi gani Rais Karume ameweza kutekeleza ahadi alizozitoa wakati wa kuomba ridhaa ya wananchi kuiongoza nchi yetu. Mafanikio hayo ni kama ifuatavyo:-

1. Mradi mkubwa wa Malaria,
2. Ujenzi wa barabara mijini na vijijini,
3. Usambazaji wa maji safi mijini na vijijini,
4. Usambazaji wa umeme mijini na vijijini,
5. Ujenzi wa Madarasa,
6. Uchapishaji wa vitabu,
7. Mradi wa kupeleka umeme Pemba kutoka Tanga,
8. Mradi wa maji katika Manispaa ya Zanzibar,
9. Malipo ya Wastaafu,

10. Mikopo ya Benki kwa Wafanyakazi,
11. Kulipa madeni ya Benki ya Watu wa Zanzibar,
12. Kulipa madeni ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii,
13. Mradi wa matengenezo ya uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Zanzibar.
14. Ununuzi wa vifaa vya kisasa katika Hospitali ya Mnazimmoja,
15. Ujenzi wa Uwanja wa Michezo wa Amani,
16. Kuimarisha Amani na Umoja kwa kupitia maridhiano na
17. Ujenzi wa Nyumba za Maendeleo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, haya si mafanikio ya kubeza hata kidogo. Rais Karume amefanya kazi ya kupigwa mfano. Bila shaka wananchi wa Zanzibar watachukua muda mrefu sana kumsahau na wataendelea kumkumbuka na uongozi wake makini na mahiri.

Tunamshukuru sana Rais Karume na tunamuomba Mwenyezi Mungu ambariki kwa wema wake.

Mhe. Spika**,** hapana shaka Serikali ya Rais Karume imefanya kazi kubwa ya kuweka misingi imara ya kukuza uchumi na maendeleo ya baadae ya Zanzibar. Kwa hiyo, Serikali itakayoingia madarakani baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu itakuwa na jukumu la kukuza uchumi na ustawi wa jamii. Kutokana na umakini wa mgombea wa Urais wa Zanzibar kwa tiketi ya CCM, Dkt. Ali Mohammed Shein nina imani ataweza kuifanya kazi hiyo ya kukuza uchumi na ustawi wa jamii iwapo atachaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na wananchi.

Mhe. Spika, kwa muda mrefu vijana wa Zanzibar kama walivyo vijana wa nchi nyengine wamekuwa wakipigania kupewa nafasi za uongozi wa kisiasa. Ili kutekeleza dhamira hiyo niliamua kugombea Urais wa Zanzibar kwa tiketi ya CCM nikiwa na kauli mbiu moja ya ndoto ya matumaini kwa kizazi kipya na cha zamani. Kwa bahati mbaya kura hazikutosha. Nilishindwa katika kinyang'anyiro hicho. Najua si jambo rahisi sana kwa mwanaadamu kuwa na furaha pale anapolikosa jambo analolitamani sana. Lakini lazima tujifunze kuikubali hali ya mambo ilivyo. Nilishindwa kwa sababu Mwenyezi Mungu hakupenda iwe hivyo. Mwenyezi Mungu anasema hivi Bismilllahi rahman rahim, **"Anapotaka jambo liwe husema liwe na linakuwa"**. Vile vile Mwenyezi Mungu anasema, **" Binaadamu anapanga na Mungu anapangua"** mimi nilipanga Mwenyezi Mungu amepangua**.** Kwa mnasaba huu nawaomba marafiki wapenzi na watu wote walionipigania nishinde waukubali ukweli huu. *(Makofi)*

Nawaomba wawe na subira hasa vijana. Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wanaosubiri. Mwanamuziki wa Ragae Marehemu Bob Marley alisema, *"Get up stand-up, do not loose the fight"* simameni msikate tamaa kuweni na moyo**.** Nawaomba vijana wakumbuke kuwa jambo ambalo halikuwezekana leo linaweza kutokea kesho. CCM ni kama jahazi – jahazi hili leo limembeba Dkt. Sheni, siku moja linaweza kumbeba Nahodha au mtu mwengine atakayebahatika. Kwa mantiki hiyo sisi tulio katika chama tawala tunao wajibu mkubwa sana kwa nguvu zetu zote mgombea aliyeteuliwa na CCM. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika kunyang'anyiro cha kugombea Urais wa Zanzibar kwa tiketi ya CCM nimejifunza jambo moja kubwa sana. Watu wote wanaofanikiwa katika maisha wanakutana na mitihani mikubwa sana katika maisha. Mafanikio hayaji kama mvua yapatikana kwa bidii kubwa na pengine muda mrefu. Mwandishi mmoja maarufu wa vitabu vya uongozi bwana Rubi Shamal mwenye asili ya India lakini anaishi Marekani alisema maneno haya na fikiri vijana wenzangu na wazee wayatafakari maneno haya.

"There are many paths to the mountain top. We all travel different roads to our ultimate destinations. For some of us the path is rockier than others. But no one reaches the end without facing some form of adversity. So rather than fight it why not accept as the part of life? You would not have the wisdom you now possess were it not for the setbacks you have faced, the mistakes you have made and the suffering you have endured. Once and for all, come to realize that pain is a teacher and failure is the highway to success".

Kwa lugha yetu ya kiswahili anasema. " *Kuna njia nyingi kufikia juu ya mlima tunasafiri kupitia njia tofauti kuelekea kule tunakokwenda kwa baadhi yetu njia huyo inakuwa na majabali na milima, lakini hakuna mtu anayesikia huko alikokusudia kwenda bila ya kukutana na mitihani mbali mbali njiani, badala ya kuukubali ukweli wa mambo ulivyo unavyoshindwa hakuna haja ya kupigana usingekuwa na busara na hekima uliyokuwa nayo hivi sasa kama hukupambana na mateso mbali mbali katika maisha yako, na sasa tunakubali kwamba maumivu, matatizo ni mwalimu na kushindwa kufikia yale uliyoyatarajia ni barabara kuelekea mafanikio siku zijazo".*

Mhe. Spika, katika kipindi changu cha kuwa Kiongozi wa shughuli za Serikali Barazani nimejifunza mengi. Waheshimiwa Wawakilishi wamekuwa walimu wangu. Baraza la Wawakilishi limekuwa Chuo changu Kikuu cha Maisha *(The University of Life).* Nimejifunza mengi kutokana na michango ya wajumbe. Pengine nimejifunza mambo ambayo nisingeweza kujifunza darasani. Nawashukuru Wajumbe kwa kunipa msaada mkubwa sana. Nitawakumbukeni Daima. Kwa kuwa ninaamini kwa dhati ya moyo wangu Mwenyezi Mungu huwalipa wanaadamu kwa kila kazi njema iliyotukuka waliyoifanya hapa

duniani, natumai san asana nitarudi Barazani Inshaallah kwa kupitia jimbo langu. *(Makofi)*

Nitawatumikia wananchi wa Zanzibar nikiwa ndani ya serikali au nje ya serikali kwani huo ndio wajibu wangu kuitumikia Zanzibar kama aliyekuwa Rais wa Marekani alivyosema Joneth Kenedy usiulize nchi yako itakufanyia nini bali uliza nchi yako utaifanyia nini nchi yangu nimeifanyia mengi, nimefika hapa kwa ajili ya nchi yangu sasa umefikia wakati kutafuta njia ya kutumikia nchi yangu ili kufikia upeo huo wa matarajio. Mungu akubarikini nyote kwa wema wenu na msaada wenu mkubwa kwangu na imani mliyonionesha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu liahirishwe hadi tarehe 09 Agosti mwaka 2010 saa 3.00 asubuhi.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza Mungu akubarikini sana. *(Makofi)*

(Saa 9.50 asubuhi Baraza liliahirishwa hadi tarehe 9/08/2010
Saa 3.00 asubuhi)